



United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

TAARIFA KWA VYOMBA VYA HABARI

Kuadhimisha Safari Yetu: Maonyesho ya Mashujaa na Mapambano yetu ya kupata Uhuru yazinduliwa Makumbusho ya Taifa- Nyumba ya Utamaduni, Tanzania

UNESCO kwa kushirikiana na Washirika wa Mradi unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU), kwa lengo ya kuendeleza juhudi za Uhifadhi wa Hifadhi ya Urithi Tanzania, hususani ya Ukombozi wa Africa, utafanya maonyesho kutoka tarehe 27 Oktoba 2017 kwa mwezi mmoja kwenye Makumbusho ya Taifa- Nyumba ya Utamaduni, Dar es Salaam, Tanzania.

Uzinduzi wa maonyesho unaendana na kumbukumbu ya kimataifa ya Siku ya Ulimwengu ya Urithi wa Picha na Sauti iliyobeba mada ya *kugundua, kukumbuka na kushiriki*, mwaka huu. Kwa njia ya kuhifadhi urithi wa picha na sauti, jitahada hizi hutoa ufahamu wa kipekee ya siku za nyuma kama msingi wa kuangalia na kujipanga na maendeleo ya siku zijazo. Urithi huu unaleta kumbukumbu na ushuhuda, ujuzi na mawazo, kwa njia ambazo ni wazi na zinaweka misingi ya ufahamu bora na majadiliano kati ya vizazi, pamoja na kati ya jamii. Kuunganisha urithi wa zamani na sasa, utajiri huu ni sehemu ya historia yetu ya kawaida, na lazima ihifadhiwe na kushirikiana kama taifa kuzalisha mali, uvumbuzi na ubunifu mahiri.

Filamu, vifaa vyenye sauti, redio na televisheni – hizi nyaraka ni muhimu kwa ajili ya kulinda urithi, na kutupa nafasi ya kuangalia historia yetu na ya wengine katika hadithi kubwa kama wosia ya binadamu wote, kwa misingi ya heshima na uvumilivu. Kumbukumbu hizi ziko hatarini kupotea, na vinatutoka kwa njia nyingi, pamoja na kuoza. Ndiyo sababu UNESCO inafanya kazi na Serikali duniani kote kulinda urithi wa picha na sauti kama chanzo cha wote kushiriki katika maendeleo- kwa kuwezesha wanawake na wanaume leo na kesho kugundua, kukumbuka na kugawana urithi ambao unatuputa utambulisho wetu.

Katika mfumo wa Mradi huu, haya maonyesho, kati ya shughuli nyingine, inalenga kuchangia kuhakikisha uendelevu wa uhifadhi bora wa nyaraka za urithi kwa kuongezeka kwa uwajibikaji, upatikanaji na udhibiti wa urithi huu muhimu. Maonyesho yatasaidia kuongeza ufahamu, uonekano na ufikiaji wa urithi wa kumbukumbu, hususani yale yanayohusishwa na mapambano ya uhuru, kwa kuelekezea msisitizo juu ya mchango wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mapambano haya, hasa kwa vijana.

Taasisi za Taifa wanaoshiriki katika Mradi huu ni Shirika la Utangazaji Tanzania, Makumbusho ya Taifa ya Tanzania, Kumbukumbu za Taifa za Tanzania na Mfuko wa Mwalimu Nyerere kwa kushirikiana na Programu ya Urithi wa Afrika katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

UNESCO Dar Office, Tanzania | Nancy Kaizilege | +255 789 288 730| nk.kaizilege@unesco.org